

MAHAKAMA kuu vuga imempeleka chuo cha mafunzo miaka 2, kijana Ismail Haji Khatib kwa kosa la usafirishaji dawa haramu kinyume na kifungu cha 50 na 61.cha sheria ya kuzuia rushwa na uhujumu wa uchumi Zanzibar no 1 ya mwaka 2012.

Mbele ya Mh Jaji wa mahakama kuu vuga Abdul Hakim Ameri Issa amehukumiwa kwa kosa hilo na kutakiwa kulipa faini ya sh milioni 2 za kitanzania na akishindwa kulipa faini hiyo, kwenda chuo cha mafunzo miaka miwili.

Inadaiwa kuwa kijana Ismail Haji Khatib siku ya tarehe 15/2/2018 majira ya saa 4:50 za asubuhi huko welezo wilaya ya magharib B mkoa wa Mjini Magharib bila ya halali amekutwa akisambaza parket 250 za unga unaosadikiwa kuwa ni dawa za kulevya aina ya heroin wenye uzito 3.9075g kwa kila packet moja ambao umefungwa katika foil paper kitendo ambacho nikosa kisheria